**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

**(PPRA)**

# MWONGOZO WA JUMLA WA UNUNUZI WA UMMA ENDELEVU, 2025

**JANUARI 2025**

*Tarehe ya Kuanza Kutumika: 23 Januari 2025*

**MWONGOZO WA JUMLA WA UNUNUZI WA UMMA ENDELEVU, 2025**

| Umeidhinishwa na | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Bodi ya Wakurugenzi | Mkurugenzi Mkuu | | 22 Januari 2025 |

**Umetolewa na:**

*Mkurugenzi Mkuu,*
*Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma,*
*Tambukareli Dodoma,*
*3 Mtaa wa Ununuzi,*
*S.L. P 2865,*
*41104 Dodoma, TANZANIA*
*Barua pepe: dg@ppra.go.tz*
*Simu: +255 (0) 26 296 3854*
*Tovuti: https://www.ppra.go.tz*

**YALIYOMO**

ORODHA YA VIFUPISHO ..... iii
TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA ..... iv
SEHEMU YA KWANZA: MASHARTI YA JUMLA ..... 1
Dibaji ..... 1
Lengo ..... 2
Matumizi ya Mwongozo ..... 2
Masharti Wezeshi ya Ununuzi wa Umma Endelevu katika Mfumo wa Kisheria ..... 3
Mamlaka ya PPRA kutoa Miongozo ya Ununuzi wa Umma Endelevu ..... 3
Tafsiri ya maneno ..... 4
Ununuzi wa Umma Endelevu ..... 6
Nguzo za Ununuzi wa Umma Endelevu ..... 6
Wadau Muhimu na Majukumu yao katika Utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu ..... 12
SEHEMU YA PILI: KUJUMUISHA UNUNUZI WA UMMA ENDELEVU KATIKA MCHAKATO WA UNUNUZI ..... 20
Ununuzi wa Umma Endelevu kwenye Mzunguko wa Ununuzi ..... 20
Utafiti wa Soko ..... 21
Uandaaji wa Bajeti ..... 22
Upangaji wa Ununuzi ..... 23
Zabuni ..... 24
Tathmini ya Zabuni ..... 27
Utoaji wa Tuzo ..... 28
Usimamizi wa Mikataba ..... 28
Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo ..... 32
ORODHA YA MAJEDWALI ..... 33

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| $CO_2$ | - | Hewa Ukaa |
| EWURA | - | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| GCLA | - | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali |
| GN | - | Tangazo la Jumla |
| LCC | - | Gharama za Mzunguko wa Maisha |
| LCA | - | Tathmini ya Mzunguko wa Maisha |
| NEMC | - | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| NEEC | - | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| NeST | - | Mfumo wa Kieletroniki wa Ununuzi wa Umma wa Tanzania |
| OSHA | - | Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi |
| PEs | - | Taasisi Nunuzi |
| PPA | - | Sheria ya Ununuzi wa Umma |
| PPRA | - | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma |
| SDG's | - | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SEA/SH | - | Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia / Ukatili wa Kijinsia |
| SPP | - | Ununuzi wa Umma Endelevu |
| STDs | - | Nyaraka Sanifu za Zabuni |
| SMEs | - | Biashara Ndogo na za Kati |
| TBS | - | Shirika la Viwango Tanzania |
| TMDA | - | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania |

## TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA

| | |
|---|---|
| **Jina la Nyaraka** | Mwongozo wa Jumla wa Ununuzi wa Umma Endelevu, 2025 |
| **Toleo** | Toleo la Kwanza, Januari 2025 |
| **Namba ya Nyaraka** | PPRA/PSCD/MPS/25/07 |
| **Jukumu** | Menejimenti, Taasisi Nunuzi |
| **Imeandaliwa na** | Menejimenti |
| **Uidhinishwaji wa Kwanza, (Toleo la Kwanza)** | Bodi, Januari 2025 |
| **Matumizi** | Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Menejimenti |
| **Dhumuni** | Kutoa mwongozo kwa Taasisi Nunuzi kuhusu utekelezaji wa ununuzi wa umma endelevu katika hatua zote za mzunguko wa ununuzi na kubainisha mbinu bora za ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa njia endelevu |
| **Ni sehemu ya** | Miongozo ya Ununuzi wa Umma |
| **Nyaraka Nyingine zinazohusiana** | Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 |
| **Usambazaji** | Bodi, Menejimenti, Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, Afisa Masuuli, Taasisi Nunuzi na Wazabuni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SEHEMU YA KWANZA: MASHARTI YA JUMLA** | | | |
| 1. | **Dibaji** | 1.1 | Mnamo mwaka 2015, Umoja wa Mataifa ulipitisha Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Ajenda hii iliweka Malengo kumi na saba ya Maendeleo Endelevu yenye shabaha na viashiria mbalimbali. Ajenda ya 2030, miongoni mwa mambo mengine, inalenga kutokomeza umaskini miongoni mwa nchi wanachama na kuhakikisha kuwa mataifa hayo yanakwenda katika maendeleo endelevu.<br><br>Kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kumi na saba, Lengo la 12 ni mahususi kuhakikisha mifumo endelevu ya matumizi na uzalishaji. Chini ya lengo hili, Shabaha ya 12.7 inalenga kukuza mbinu za ununuzi wa umma ambazo ni endelevu, kwa mujibu wa sera na vipaumbele vya kitaifa, na utekelezaji wake hupimwa kupitia Kiashiria 12.7.1 ambacho kinalenga kuweka idadi ya nchi zinazotekeleza sera na mipango kazi ya Ununuzi wa Umma Endelevu *(SPP).* |
| | | 1.2 | Kufuatia Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, baada ya mwaka 2015, Tanzania iliridhia Ajenda 2030 na kuyajumuisha Malengo ya Maendeleo katika Mipango yake ya Maendeleo ya Kati na ya Muda Mrefu. Kuridhia huko kwa Ajenda 2030 kulisababisha mapitio ya mfumo wa kisheria wa ununuzi ambapo pamoja na mambo mengine ilijumuisha masharti kuhusu ununuzi wa umma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | endelevu unaoendana na Shabaha 12.7 chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu inayolenga kukuza mbinu za ununuzi wa umma endelevu. |
| | | 1.3 | Kwa hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeandaa huu *Mwongozo wa Jumla wa Ununuzi wa Umma Endelevu, 2025* ili kutoa mwongozo kwa vitendo kwa Taasisi Nunuzi *(PEs)* kujumuisha mahitaji ya uendelevu katika mzunguko wao wa ununuzi. |
| | | 1.4 | Hivyo basi, ili kufikia madhumuni ya uendelevu katika ununuzi wa umma, Taasisi Nunuzi zinapaswa kuzingatia kikamilifu Mwongozo huu katika shughuli zao za ununuzi za kila siku. |
| 2. | **Lengo** | 2.1 | Kutoa mwongozo kwa Taasisi Nunuzi kwenye utekelezaji wa ununuzi wa umma endelevu katika mzunguko mzima wa ununuzi na kuelezea mbinu bora za kununua bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa njia endelevu. |
| 3. | **Matumizi ya Mwongozo** | 3.1 | Mwongozo huu utatumika kwa Taasisi Nunuzi zote zinazotumia fedha za umma kufanya ununuzi endelevu wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni za Ununuzi wa Umma. |
| | | 3.2 | Miongozo iliyo hapa chini itakamilisha utekelezaji wa mwongozo wa jumla wa ununuzi wa umma endelevu uliotolewa chini ya Mwongozo huu:-<br>(a) Mwongozo wa ununuzi wa umma endelevu kuhusu matumizi ya utaratibu wa upendeleo;<br>(b) Mwongozo wa ununuzi wa umma endelevu kuhusu ushiriki wa makundi maalum katika ununuzi wa umma; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (c) Mwongozo wa ununuzi wa umma endelevu kuhusu wahitimu wanaojifunza kwa vitendo katika ununuzi wa umma;<br>(d) Mwongozo wa ununuzi wa umma endelevu kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zilizotambuliwa kama vipaumbele maalum;<br>(e) Mwongozo wa Ushirikishaji wa Jamii. |
| 4. | **Masharti Wezeshi ya Ununuzi wa Umma Endelevu katika Mfumo wa Kisheria** | 4.1 | Ununuzi wa umma endelevu nchini Tanzania umeelezwa chini ya Kifungu cha 5 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Sheria inataka ununuzi wote na uondoshaji mali kwa njia ya zabuni kufanywa kwa namna itakayowezesha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha na kuongeza uadilifu, ushindani, uwajibikaji, **uendelevu,** uchumi, ufanisi na uwazi.<br>Sheria pia inazitaka Taasisi Nunuzi, katika kutekeleza wajibu wao, kufikia viwango vya juu vya usawa, kuzingatia fursa sawa kwa wazabuni wote, haki kwa pande zote, kukuza viwanda vya ndani, **maendeleo endelevu**, uhifadhi wa mazingira, na uhitaji wa kupata thamani halisi ya fedha kulingana na bei, ubora na muda wa utekelezaji, kwa kuzingatia vigezo msawazo na sifa zilizoainishwa. |
| 5. | **Mamlaka ya PPRA kutoa Miongozo ya Ununuzi wa Umma Endelevu** | 5.1 | Kifungu cha 130 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kinatoa mamlaka kwa PPRA kutoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa matakwa ya sheria. Kupitia Kanuni ya 3 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024, PPRA inawajibika kuandaa Mwongozo wa Jumla wa Ununuzi wa Umma Endelevu ili kuziwezesha Taasisi Nunuzi kujumuisha mahitaji ya Ununuzi wa Umma Endelevu katika ununuzi wao. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | **Tafsiri ya maneno** | 6.1 | **Mamlaka** maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma.<br><br>**Alama za Mazingira** maana yake ni uthibitisho unaotolewa kwa bidhaa, huduma, au kampuni ambazo zimekidhi vigezo mahususi vya utendaji wa kimazingira. Uthibitisho huo unatoa kwa watumiaji taarifa kuhusu athari za kimazingira za bidhaa au huduma, zinazowasaidia kufanya machaguo endelevu zaidi.<br><br>**Ununuzi wa Umma wa Kijani** Ni mchakato ambao mamlaka za umma na wakala wa serikali huhitaji kufanya ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi za ujenzi zenye athari ndogo kimazingira katika mzunguko mzima wa maisha yake.<br><br>**Mzunguko wa Maisha** maana yake ni hatua mfululizo na zinazohusiana za mfumo wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma, kuanzia upatikanaji wa malighafi au uzalishaji kutoka rasilimali asilia hadi uondoshaji wa mwisho.<br><br>**Gharama za Mzunguko wa Maisha** Ni mbinu ya kukokotoa gharama za bidhaa, kazi za ujenzi na huduma katika mzunguko wake mzima wa maisha.<br><br>**Tathmini ya Mzunguko wa Maisha** Ni mchakato wa hatua kwa hatua unaotumika kutathmini athari za kimazingira zinazohusiana na hatua zote za mzunguko wa maisha ya bidhaa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Taasisi Nunuzi** maana yake ni taasisi ya umma na taasisi nyingine yeyote au kitengo kilichoanzishwa na kupewa mamlaka na Serikali kufanya shughuli za umma. |
| | | | **Ununuzi** maana yake ni kununua, kupanga, kukodisha, kununua kwa kukodisha au kupata bidhaa, kazi za ujenzi au huduma yoyote kwa Taasisi Nunuzi na inajumuisha kazi zote zinazohusisha upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma , ikijumuisha kutambua na kuandaa mahitaji, uchaguzi na mwaliko wa wazabuni, maandalizi ya mikataba, tuzo na usimamizi wa mikataba.<br><br>**Maendeleo Endelevu** maana yake ni maendeleo yanayokidhi mahitaji ya sasa bila kuhatarisha uwezo wa vizazi vijavyo kukidhi mahitaji yao wenyewe.<br><br>**Ununuzi Endelevu** maana yake ni ununuzi unaotoa matokeo chanya zaidi katika uchumi, jamii na mazingira katika mzunguko mzima wa maisha.<br>**Makundi Maalam** inajumuisha wanawake, vijana, wazee, na watu wenye ulemavu.<br><br>**Zabuni** maana yake ni ofa, pendekezo au ofa ya bei inayowasilishwa na muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mshauri elekezi kutika kuitikia ombi la Taasisi Nunuzi.<br><br>**Mzabuni** maana yake ni mtu yeyote wa asili au wa kisheria, au kundi la watu kama hao, anayeshiriki au anayekusudia kushiriki katika mchakato wa ununuzi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kwa lengo la kuwasilisha zabuni kwa ajili ya kuingia mkataba, na inajumuisha muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, mtoa huduma au mnunuzi wa mali.<br><br>**Thamani halisi ya Fedha** maana yake ni manufaa makubwa yanayopatikana kwenye bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zilizonunuliwa na rasilimali zilizopo ikilinganishwa na gharama zilizotumika. |
| 7. | **Ununuzi wa Umma Endelevu** | 7.1 | Ununuzi wa Umma Endelevu maana yake ni mchakato ambao Taasisi Nunuzi hukidhi mahitaji yao ya bidhaa, kazi za ujenzi, au huduma kwa njia inayoipatia thamani halisi ya fedha kwa kuzingatia mzunguko mzima wa maisha inayohusisha kuzalisha manufaa si tu kwa shirika, bali pia kwa jamii na uchumi, huku ikipunguza kwa kiwango kikubwa, na ikiwezekana, kuepusha kabisa, athari hasi kwa mazingira, uchumi na ustawi wa jamii. |
| | | 7.2 | Ununuzi endelevu unahusisha kuangalia zaidi ya mahitaji ya muda mfupi na kuzingatia athari za muda mrefu za kila mradi na ununuzi. Taasisi Nunuzi zinapaswa kukidhi mahitaji yao ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma sio kwa manufaa binafsi, bali kwa mtazamo wa kuongeza manufaa halisi kwao na kwa dunia kwa ujumla. |
| 8. | **Nguzo za Ununuzi wa Umma Endelevu** | 8.1 | Ununuzi wa Umma Endelevu ni mbinu ya kimkakati inayokuza ujumuishaji wa nguzo za maendeleo endelevu, yaani, maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kijamii na uhifadhi wa mazingira. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 8.2 | Taasisi Nunuzi zinapaswa kuzingatia maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kijamii na uhifadhi wa mazingira katika ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma kama ifuatavyo:- |
| | | 8.3 | **Mazingatio ya Kiuchumi**<br>a) Mazingatio ya kiuchumi katika Ununuzi wa Umma Endelevu yanalenga kupata ufanisi wa kifedha na kuchochea ukuaji wa uchumi huku yakihakikisha uendelevu wa ununuzi wa umma. Yanaakisi gharama za ununuzi wa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zinazohusiana moja kwa moja na mchakato wa ununuzi na hatua kuu za mzunguko wake wa maisha (mfano: uendeshaji, urejelezaji/utumiaji) ili kufikia uchumi wa juu, ufanisi, na matumizi bora ya bajeti;<br><br>b) Katika kuzingatia suala la kiuchumi Taasisi Nunuzi zitapaswa:-<br>i) Kuhakikisha kuzingatiwa kwa misingi ya uendelevu wa kiuchumi kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazonunuliwa katika hatua zote za utendaji wa ununuzi wa umma;<br>ii) Kutoa kipaumbele kwa maamuzi ya ununuzi yanayohakikisha bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazonunuliwa zinakidhi mahitaji ya taasisi za umma na wadau;<br>iii) Kufanya tathmini ya gharama za awali za bidhaa, kazi za ujenzi au huduma na gharama zake za muda mrefu kama vile uendeshaji, matengenezo, uondoshaji, na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | athari zozote zinazoendana kimazingira au kijamii;<br>iv) Kutoa kipaumbele kwa ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kutoka kwa wazabuni wa ndani na biashara ndogo na za kati ili kukuza ukuaji wa uchumi wa kikanda na kitaifa katika mkoa na taifa; na<br>v) Kutekeleza Miongozo ya Mpango wa Upendeleo inayotolewa na PPRA ili kuhakikisha wazabuni wa ndani wanapewa fursa sawa kushindana katika zabuni za kusambaza bidhaa, ufanyaji kazi za ujenzi au kutoa huduma kwa kujumuisha wazabuni wa ndani na biashara ndogo na za kati katika michakato ya ununuzi. |
| | | 8.4 | **Mazingatio ya Kijamii**<br>a) Mazingatio ya kijamii katika Ununuzi wa Umma Endelevu yanahusisha uunganishwaji wa malengo ya kijamii katika maamuzi ya ununuzi ili kuhakikisha bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zinazonunuliwa zinatoa manufaa chanya ya kijamii. Ununuzi wa Umma Endelevu unalenga kutumia nguvu ya ununuzi ya serikali kukuza usawa wa kijamii, haki za wafanyakazi, na ustawi mpana wa jamii.<br><br>b) Katika kuzingatia masuala ya kijamii Taasisi Nunuzi zitapaswa: -<br><br>i) Kukuza fursa za ajira, na ujuzi kwa nguvu kazi, mazingira bora ya kazi, ushirikishaji wa kijamii, usawa wa kijinsia na kutokubagua, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | upatikanaji, ubunifu kwa wote, biashara yenye maadili, na uzingatiaji wa haki za kijamii na za kazi;<br><br>ii) Kuchagua bidhaa na huduma zinazotoa matokeo chanya ya kijamii, na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo endelevu;<br><br>iii) Sio tu kupendelea kununua kwa bei ya chini au thamani halisi ya fedha, vile vile kuhakikisha ununuzi unatoa manufaa ya kijamii na kuzuia au kupunguza athari mbaya za kijamii wakati wa utekelezaji wa mkataba;<br><br>iv) Kufuatilia masharti ya mkataba ya sheria za lazima za kijamii na wafanyakazi katika utekelezaji wa mkataba wa ununuzi;<br><br>v) Kutoa upendeleo kwa makundi maalum na biashara ndogo na za kati kama ilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Makundi Maalum uliotolewa na Mamlaka; na<br><br>vi) Kuhakikisha watu wa ndani wananufaika na fursa za ununuzi ili kuwasaidia kupata faida ya kiushindani katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. |
| | | 8.5 | **Mazingatio ya Kimazingira**<br>a) Ununuzi endelevu kimazingira una maana ya mkakati wa tahadhari kuhusu ununuzi unaofanywa na Taasisi Nunuzi kuhusiana na bidhaa na huduma zenye utendaji bora katika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kulinda mazingira. Hii pia inamaanisha kununua kulingana na mahitaji na kuepuka ziada au upotevu.<br><br>b) Katika kuzingatia suala la mazingira Taasisi Nunuzi zitapaswa: -<br><br>i) Kuzingatia athari za bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazonunuliwa kwenye mazingira na usalama wa afya ya binadamu;<br><br>ii) Kuzingatia sheria na kanuni za mazingira;<br><br>iii) Kuzingatia ununuzi endelevu kimazingira kwa manufaa ya mazingira wakati wote wa mchakato wa ununuzi;<br><br>iv) Kuzingatia viwango vya mazingira, uthibitishaji na uwekaji lebo kwa “Bidhaa au Huduma za Kipaumbele za Ununuzi wa Umma Endelevu” zilizoainishwa na Mamlaka na kuingizwa kwenye mfumo wa *NeST*;<br>v) Wakati wa ununuzi wa bidhaa au huduma ambazo hazijajumuishwa kwenye “Bidhaa au Huduma za Kipaumbele za Ununuzi wa Umma Endelevu” kuzingatia bidhaa na huduma ambazo zina athari ndogo kwa mazingira au zile ambazo zina mbadala rafiki kwa mazingira ambazo zinapatikana kirahisi na zisizoongeza gharama za ziada. Bidhaa, kazi za ujenzi, au huduma zitakazonunuliwa ni zile zenye athari ndogo katika mazingira kwa upande wa mabadiliko ya tabia ya nchi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | au usimamizi wa taka, ikijumuisha kuboresha ufanisi wa nishati katika majengo ya umma mapya na yaliyokarabatiwa;<br><br>vi) Kujumuisha sharti la uthibitishaji au viwango vya kuhifadhi mazingira katika nyaraka za zabuni;<br><br>vii) Kufanya Tathmini ya Mzunguko wa Maisha wakati wa mchakato wa tathmini ya zabuni kwa kutumia zana zilizopo kuchambua athari zinazoweza kutokea katika hatua zote za maisha ya bidhaa au huduma na kutathmini utendaji wa kimazingira wa bidhaa, huduma, na kazi za ujenzi au kumtaka mzabuni kuwasilisha taarifa ya Tathmini ya Mzunguko wa Maisha wakati wa kuwasilisha zabuni;<br><br>viii) Kutumia njia za ununuzi za majadiliano kuhamasisha mbinu za ubunifu za kimazingira na kutoa fursa za masoko kwa bidhaa za mazingira kwa wazalishaji wa ndani au watoa huduma kupata manufaa kiushindani katika ngazi ya kitaifa na kimataifa; na<br><br>ix) Kununua bidhaa na malighafi zinazozalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano kupunguza utoaji wa hewa ukaa na gharama zitokanazo na usafirishaji mrefu wa bidhaa. |
| 9. | | 9.1 | Utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu katika mchakato wa ununuzi wa umma unapaswa kuhusisha wadau muhimu ili kufanikisha malengo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Wadau Muhimu na Majukumu yao katika Utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu** | | yake. Wadau hao muhimu na majukumu yao ni kama yafuatavyo: |
| | | 9.2 | **Wizara inayohusika na Fedha**<br>Majukumu ya Wizara kwenye utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu ni:<br><br>a) Kutoa tamko la sera linalounga mkono Ununuzi wa Umma Endelevu kujumuishwa katika Sera ya Ununuzi ya Taifa;<br>b) Kutengeneza sera, sheria na kanuni za ununuzi wa umma endelevu zinazotoa mamlaka ya ujumuishaji wa uendelevu kwenye ununuzi wa umma;<br>c) Kutengeneza dira ya kitaifa ya maendeleo endelevu kwa ajili ya utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu; na<br>d) Kuwezesha rasilimali za kifedha kwa utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu. |
| | | 9.3 | **Wizara inayohusika na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**<br>a) Kushirikiana na PPRA katika kujenga uwezo kupitia ushirikishwaji, mafunzo na elimu kwa makundi maalum kuboresha ushiriki wao katika ununuzi wa umma;<br>b) Kujumuisha mahitaji ya uendelevu katika ununuzi wa umma ndani ya makundi maalum; na<br>c) Kuhakikisha masuala ya usawa wa kijinsia yanaingizwa katika Ununuzi wa Umma Endelevu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 9.4 | **Wizara inayohusika na Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu**<br>a) Kushirikiana na PPRA katika kujenga uwezo kupitia ushirikishwaji, mafunzo na elimu kwa Watu wenye Ulemavu;<br>b) Kujumuisha mahitaji ya uendelevu ya Watu wenye Ulemavu na Vijana katika ununuzi wa umma; na<br>c) Kuimarisha viwango vya kazi na mipango ya hifadhi ya jamii. |
| | | 9.5 | **Mamlaka za Udhibiti, Wakala na Taasisi za Serikali**<br>Mamlaka za udhibiti na Wakala wa kazi za ujenzi, bidhaa na huduma zina majukumu muhimu katika kukuza na kutekeleza ununuzi wa umma endelevu, ambao unalenga kujumuisha uzingatiwaji wa uendelevu wa mazingira, kijamii na kiuchumi katika maamuzi ya ununuzi wa umma. Mamlaka hizi zinahakikisha kwamba ununuzi wa umma unawiana na malengo mapana ya maendeleo endelevu kwa kuweka miongozo, viwango na taratibu za utekelezaji. Majukumu ya mamlaka za udhibiti na wakala katika muktadha wa Ununuzi wa Umma Endelevu ni kama ifuatavyo:<br><br>(a) **Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)**<br>i) Kutambua na kuchapisha katika *NeST* orodha ya kazi za ujenzi, bidhaa, na huduma za kipaumbele cha Ununuzi wa Umma Endelevu kwa kushirikiana na wadau husika; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ii) Kutengeneza Miongozo mahususi ya Ununuzi wa Umma Endelevu kwa bidhaa na huduma za kipaumbele zilizoainishwa, kutoa maelekezo na viwango vya wazi ili kuongoza utelekezaji wa ununuzi endelevu;<br><br>iii) Kujumuisha masuala ya uendelevu wa kijamii, kiuchumi na kimazingira katika Nyaraka Sanifu za Zabuni;<br><br>iv) Kutengeneza zana za utekelezaji wa ununuzi (Miongozo ya Mafunzo, Miongozo, Fomu n.k.) ili kusaidia utekelezaji bora wa Ununuzi wa Umma Endelevu;<br><br>v) Kuweka na kuhifadhi kanzidata ya vigezo vya uendelevu;<br><br>vi) Kujenga uwezo wa Ununuzi wa Umma Endelevu kupitia ushirikishwaji, mafunzo, na programu za elimu kwa wadau;<br><br>vii) Kufuatilia upitishwaji na utekelezaji wa Miongozo ya Ununuzi wa Umma Endelevu, kuhakikisha uzingatiwaji na ufuatiliaji wa maendeleo dhidi ya malengo endelevu katika ununuzi wa umma;<br><br>viii) Kushirikisha soko kwa kuongeza uelewa kuhusu utekelezaji wa ununuzi endelevu kupitia programu zinazolenga kusaidia wadau kujiandaa kwa mabadiliko yajayo na kuendana na mahitaji ya uendelevu katika zabuni zao; |


| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ix) Kuingia hati ya makubaliano na taasisi nyingine za usimamizi ili kuharakisha utekelezaji wa ununuzi endelevu ndani ya Taasisi Nunuzi; na<br><br>x) Kuandaa na kufanya mapitio ya mpango kazi wa utekelezaji wa Ununuzi wa Umma Endelevu.<br>(b) **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**<br>i) Kuweka viwango ambavyo wanunuzi wa umma wanatakiwa kufuata wakati wa kutafuta bidhaa endelevu; na<br>ii) Kuweka miongozo ambayo inayowataka wakala wa Serikali kutoa kipaumbele kwa bidhaa zenye ufungashaji mdogo, urejelezaji au zinazotengenezwa kwa rasilimali zinazoweza kurejeshwa.<br><br>(c) **Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA)**<br>Kuthibitisha bidhaa zinakidhi viwango fulani vya afya ya mazingira, kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinanunua bidhaa salama, chakula rafiki wa mazingira na bidhaa za afya.<br><br>(d) **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**<br>i) Kutoa viwango vya ufanisi wa nishati kwa vifaa vinavyonunuliwa na taasisi za serikali, kuhimiza ununuzi wa teknolojia ya nishati mbadala au vifaa vya kuokoa maji; na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ii) Atatoa na kufuatilia viwango vinavyohusiana na matumizi ya nishati na maji, kuhakikisha kuwa bidhaa, huduma, au miundombinu inayonunuliwa na taasisi za umma inaufanisi wa nishati na inasimamiwa kwa uendelevu.<br><br>(e) **Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**<br>i) Kutengenza miongozo ya mazingira inayosaidia kuunda vigezo vya uendelevu vinavyotumika katika michakato ya ununuzi wa umma;<br><br>ii) Kutoa semina kwa wanunuzi wa umma kuhusu athari za kimazingira za maamuzi ya ununuzi na namna ya kutathmini uendelevu wa wazabuni; na<br><br>iii) Kufanya uangalizi wa tathmini za athari za mazingira kwa bidhaa, huduma, na kazi za ujenzi ili kuhakikisha kuwa hatari za kimazingira zinatambuliwa na kupunguzwa katika mchakato wa ununuzi.<br><br>(f) **Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA):**<br>i) Kuhamasisha, kuongoza, na kusimamia masharti ya usalama, afya, na ustawi wa watu waliopo kazini ikijumuisha kulinda watu zaidi ya wale watu waliokuwa kazini dhidi ya hatari za kiafya na kiusalama |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | zitokanazo au zinazohusiana na shughuli za watu waliopo kazini;<br>ii) Kutengeneza miongozo, taratibu na kanuni za utendaji kwa ajili ya kulinda uwekezaji na watu waliopo kazini dhidi ya hatari za usalama na afya zitokanazo au zinazohusiana na shughuli zinazofanywa mahali pa kazi;<br>iii) Kusajili waajiri wote au wakazi wanaokusudia kusambaza, kujenga au kuendesha maeneo ya kazi;<br>iv) Kusajili wafanyakazi wote na mitambo katika daftari la usalama na afya mahali pa kazi ambapo usalama na afya husika hufuatiliwa kwa uendelevu kupitia ukaguzi, ukaguzi wa kina, ufuatiliaji, uchunguzi na mafunzo;<br>v) Kutoa mwongozo kwa wazabuni kuzingatia mbinu bora za usalama na afya mahali pa kazi, kwa mfano Kufanya mapitio ya tathmini ya viatarishi, Kufanya mapitio ya sera ya usalama na afya; na<br>vi) Kuhamasisha mazingira salama ya kazi sambamba na malengo ya Ununuzi wa Umma Endelevu kwa kuhimiza kutumia mbinu salama za kazi ambapo leseni ya ukidhi hutolewa kwa ambao wanazingatia matakwa hayo.<br>(g) **Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA):**<br>i) Kutoa vyeti vya uchambuzi wa bidhaa zilizojaribiwa, ambazo ni muhimu kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | wanunuzi wa umma ili kuthibitisha kuwa wauzaji wa bidhaa wanakidhi viwango vya ubora vinavyohitajika; na<br><br>ii) Kutathmini athari za usalama na mazingira za kemikali zinazotumika katika bidhaa mbalimbali, kusaidia chaguzi za ununuzi salama na endelevu.<br><br>(h) **Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC):**<br>i) Kutekeleza mikakati ya kitaifa kama vile Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kama chombo cha kuwawezesha wafanyabiashara wa ndani na kukuza maendeleo endelevu; na<br>ii) Kuhamasisha sera jumuishi katika kuunda sera za ununuzi wa serikali ili kuhakikisha zinaendana na malengo ya ununuzi endelevu. |
| | | 9.6 | **Taasisi Nunuzi**<br>Taasisi Nunuzi zina majukumu yafuatayo: -<br>i) Kutekeleza sera za Ununuzi wa Umma Endelevu kwa kuhakikisha kuwa mazingatio ya uendelevu (mazingira, jamii, na uchumi) yanajumuishwa katika mchakato wa ununuzi;<br><br>ii) Kuhamasisha utekelezaji endelevu kwa wadau na kuwapatia zana na miongozo inayohitajika ili kutimiza matakwa ya Ununuzi wa Umma Endelevu; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | iii) Kujumuisha vigezo vya uendelevu katika nyaraka za zabuni na mikataba;<br><br>iv) Kutathmini zabuni kwa kuzingatia gharama za mzunguko wa maisha, athari za mazingira, na vigezo vya uwajibikaji kijamii;<br><br>v) Kufanya utafiti wa soko ili kubaini bidhaa na huduma endelevu;<br><br>vi) Kutenga rasilimali kwa ajili ya kujenga uwezo, kampeni za uelimishaji, na utekelezaji wa mikakati ya Ununuzi wa Umma Endelevu; na<br><br>vii) Kusaidia kujenga uwezo wa watumishi katika bajeti, mipango, uundaji wa vigezo vya Ununuzi wa Umma Endelevu, tathmini, uchambuzi wa gharama za mzunguko wa maisha, usimamizi wa mikataba na maeneo mengine yanayohusika na Ununuzi wa Umma Endelevu yaliyotolewa katika Mwongozo huu. |
| | | 9.7 | **Wazabuni**<br>Majukumu ya Wazabuni katika utekelezaji wa Ununuzi Endelevu wa Umma yatajumuisha yafuatayo:<br><br>i) Kuhakikisha kwamba kazi za ujenzi, bidhaa, na huduma wanazotoa zinakidhi vigezo vya uendelevu wa kiuchumi, kimazingira, na kijamii kama ilivyoainishwa katika nyaraka za zabuni na mikataba; |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>ii) Kubuni na kurekebisha mbinu zao za biashara ili kukidhi vigezo vya uendelevu vilivyowekwa na Taasisi Nunuzi;<br><br>iii) Kushirikiana na wanunuzi wa sekta ya umma katika kuendeleza bidhaa na huduma zinazokidhi viwango vya mazingira, kijamii, na kiuchumi; na<br><br>iv) Kufuata sheria na kanuni.</td></tr>
<tr><td colspan="4">SEHEMU YA PILI: KUJUMUISHA UNUNUZI WA UMMA ENDELEVU KATIKA MCHAKATO WA UNUNUZI</td></tr>
<tr><td>10.</td><td>Ununuzi wa Umma Endelevu kwenye Mzunguko wa Ununuzi</td><td>10.1</td><td>Kielelezo hapo chini kinaonyesha hatua za kawaida za ununuzi ambapo kila hatua inaaininsha mazingatio yanayohusiana na Ununuzi wa Umma Endelevu ili kuwasaidia watendaji katika kutekeleza Ununuzi wa Umma Endelevu.<br>
</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | **Utafiti wa Soko** | 11.1 | Hatua hii ni ya kwanza katika mzunguko wa ununuzi ambapo taasisi nunuzi zinapaswa kufanya utafiti na uchambuzi wa soko kuhusu upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma endelevu ili kujumuishwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka. |
| | | 11.2 | Taasisi nunuzi zinapaswa kufanya uchambuzi wa utafiti wa soko ili kuelewa kiwango cha uwezo wa usambazaji uliopo sokoni kwa sasa. |
| | | 11.3 | Taasisi nunuzi zinapaswa kuchambua hali ya soko na kulinganisha machaguo ili kuandaa utaratibu wa ununuzi unaokidhi mahitaji ambayo unajumuisha masuala ya uendelevu. |
| | | 11.4 | Utafiti wa Soko unaweza kufanyika kupitia: -<br>a) Ukusanyaji wa taarifa za bidhaa, kazi za ujenzi au huduma moja kwa moja kutoka vyanzo vinavyoaminika kama vile Chama cha Wazalishaji Tanzania, Baraza la Biashara, Viwanda, na Kilimo Tanzania, vyama vya wafanyabiashara, kampuni toka sekta binafsi, Shirika la Viwango Tanzania, Taasisi (Shirikisho) ya Sekta Binafsi Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, *AQRB* na vyanzo vingine vinavyoaminika;<br>b) Majadiliano na wazabuni watarajiwa ambao bidhaa na huduma hupatikana mara kwa mara; na<br>c) Ukusanyaji wa taarifa kutoka tovuti za kuaminika zinazohusiana na biashara na uchumi, magazeti au makala, kanzidata za wazabuni, taarifa za |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | tasnia, tafiti/dodoso na ziara za kwenye maeneo husika. |
| 12. | **Uandaaji wa Bajeti** | 12.1 | Wakati wa maandalizi ya bajeti, Taasisi Nunuzi inapaswa kuzingatia Gharama za Mzunguko wa Maisha kwa kuzingatia bei ya ununuzi, gharama za uendeshaji, gharama za utoaji hewa ukaa na gharama za mwisho wa matumizi pale inapohusika kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazonunuliwa, kwa mujibu wa **Jedwali la Kwanza** la Mwongozo huu. |
| | | 12.2 | Taasisi nunuzi itatenga fedha kwa ajili ya malipo ya wahitimu wanaofanya mafunzo kwa vitendo katika mikataba yote ya ununuzi inayotolewa kwa waendeshaji wa kiuchumi. Idadi ya wahitimu wanaofanya mafunzo kwa vitendo itazingatia Mwongozo wa Mpango wa Upendeleo uliotolewa na Mamlaka. |
| | | 12.3 | Taasisi nunuzi itazingatia viwango vya chini vya mishahara vilivyowekwa na Serikali katika mikataba yote ya ununuzi (mfano, ofa ya zabuni za huduma ya ulinzi na usafi hazipaswi kuwa chini ya viwango vya chini vya mishahara vya Serikali kwa wafanyakazi wa mzabuni). |
| | | 12.4 | Taasisi nunuzi itatenga fedha mahususi kuwekeza katika programu za kujenga uwezo wa watumishi kuhusu ununuzi wa umma endelevu. |
| | | 12.5 | Taasisi nunuzi itatenga fedha na hadidu za rejea kwa ajili ya usimamizi na ukaguzi wa mahitaji ya uendelevu wakati wa utekelezaji wa mkataba. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | **Upangaji wa Ununuzi** | 13.1 | Taasisi nunuzi zitahakikisha kuwa masuala ya ununuzi wa umma endelevu ni sehemu muhimu ya mchakato wa kupanga ununuzi. |
| | | 13.2 | Katika hatua ya kupanga, taasisi nunuzi zinapaswa kufanya tathmini ya mahitaji ili kubaini umuhimu wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma ikizingatia aina ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazohitajika, madhumuni ya kununua kila aina na kiasi kinachohitajika. |
| | | 13.3 | Taasisi nunuzi itaangalia mbadala au njia nyingine za kukidhi mahitaji (mfano: kutumia tena, kukopa, kukodisha, au iwapo mali zilizopo zinaweza kurekebishwa, kutengenezwa au kuboreshwa) kukidhi mahitaji badala ya kupanga kununua mpya. |
| | | 13.4 | Taasisi nunuzi itazingatia katika hatua ya kupanga uwezekano wa kupunguza kiasi cha bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zitazonunuliwa kwa kuchagua kununua bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazoweza kushirikiwa katika idara inapowezekana (mfano kushirikiana kutumia mashine ya uchapaji, meza, au ofisi za pamoja). |
| | | 13.5 | Taasisi nunuzi itachagua taratibu bora za ununuzi zinazohakikisha mahitaji ya kijamii yanatimizwa (mfano: kuzuia zabuni kwa eneo la kijiografia, mkoa n.k). |
| | | 13.6 | Taasisi nunuzi inaweza kutumia loti au kugawa zabuni kwa mikataba iliyohifadhiwa kwa wanawake, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalum. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 13.7 | Taasisi nunuzi itachunguza iwapo bidhaa, kazi ujenzi au huduma zinazohitajika zinafanana katika idara mbalimbali kama zinaweza kuunganishwa na kununuliwa chini ya Mikataba Maalumu. |
| | | 13.8 | Taasisi nunuzi itahifadhi mikataba kwa makundi maalum na kujenga uwezo kwa wazabuni wa ndani kama ilivyoainishwa kwenye miongozo husika iliyotolewa na Mamlaka. |
| 14. | **Zabuni** | 14.1 | Hatua hii katika mzunguko wa ununuzi inajumuisha kuandaa vigezo msawazo vya kiufundi na vigezo vya tathmini ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zitakazonunuliwa pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni. |
| | | 14.2 | Taasisi nunuzi itaandaa vigezo vya ununuzi wa umma endelevu vinavyoendana na malengo ya uendelevu ya taasisi, kwa kujumuisha mazingatio ya kiuchumi, kimazingira na kijamii katika mchakato wa kufanya maamuzi sambamba na Miongozo Maalum ya Kimataifa na Kitaifa inayotolewa na Mamlaka mara kwa mara. |
| | | 14.3 | Taasisi nunuzi zitaandaa nyaraka za zabuni zitakazojumuisha vigezo msawazo na vigezo vya tathmini vilivyoelezwa kama ifuatavyo:<br><br>a) Taasisi nunuzi itaweka sharti linalowataka wazabuni kushirikisha watu au kampuni za ndani, au kutumia bidhaa zinazozalishwa, kuchimbwa au kutengenezwa ndani ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyobainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango wa Upendeleo uliotolewa na Mamlaka; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | b) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa wafanyakazi wote wa wazabuni watakaofanya kazi za ujenzi au kutoa huduma lazima wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala ya mazingira na kijamii;<br><br>c) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa upendeleo utatolewa kwa mzabuni anayeaminika, anayetoa suluhisho bunifu na endelevu linalokidhi mahitaji ya ununuzi ya taasisi nunuzi;<br><br>d) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa upendeleo utatolewa kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zinazotumia nishati kidogo au vyanzo vya nishati vinavyoweza kurejelezwa na zinazotumia rasilimali kwa ufanisi zaidi, au zenye utoaji mdogo wa hewa ukaa;<br><br>e) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa mzabuni anayekidhi viwango vya kitaifa au kimataifa vilivyotambulika atapewa upendeleo katika mchakato wa tathmini;<br><br>f) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa upendeleo utatolewa kwa wazabuni wanaoofa kusambaza bidhaa zinazotengenezwa au kuzalishwa kwa kutumia malighafi zinazoweza kurejelewa na kutumia vifungashio vilivyopunguzwa, vinavyoweza kurejelewa au kutumika tena;<br><br>g) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa upendeleo utatolewa kwa wazabuni wanaotoa bidhaa zisizo na kemikali hatarishi na uchafuzi, ili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kuchangia mazingira salama na yenye afya zaidi;<br><br>h) Taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa wazabuni lazima waonyeshe ukidhi wa sheria za kazi, kama vile ujira stahiki, kuzingatia sera za kupinga ajira kwa watoto, ajira za kulazimishwa, na kufuata taratibu za usalama na afya mahali pa kazi;<br><br>i) Pale inapohusika, taasisi nunuzi itaweka sharti kuwa wazabuni wote katika mikataba yao ya ununuzi wanapaswa kuajiri watu wenye mahitaji maalum katika kutekeleza kazi za ujenzi au kutoa huduma;<br><br>j) Taasisi nunuzi inaweza kujumuisha masharti ya utendaji au ufanisi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma katika nyaraka za zabuni bila kuweka maelezo ya kina ya vigezo msawazo vya kiufundi;<br><br>k) Taasisi nunuzi itaweka katika nyaraka za zabuni utaratibu wa kuhakikisha kuwa vigezo vya uendelevu vilivyoainishwa kwenye zabuni vimezingatiwa (mfano: taarifa za maabara, vipimo, au ushahidi wa kupitia nyaraka); na<br><br>l) Taasisi nunuzi itaweka kwenye nyaraka za zabuni sharti la kuwasilisha mpango wa usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 14.4 | Taasisi nunuzi itatumia masharti ya vigezo msawazo vilivyowekwa kutathmini ukidhi wa wazabuni. |
| 15. | **Tathmini ya Zabuni** | 15.1 | Hatua hii inahusisha kufanya tathmini na kuandaa taarifa ya tathmini ya zabuni. Taasisi Nunuzi inapaswa kutathmini zabuni kulingana na vigezo vya tathmini na utoaji wa tuzo vilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni. |
| | | 15.2 | Taasisi Nunuzi inapaswa kuzingatia mwongozo wa vitendo uliotolewa hapa chini: -<br>a) Kutathmini ubora wa suluhisho endelevu lililopendekezwa kwa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma;<br>b) Kutathmini sifa za uendelevu za wazabuni na rekodi zao kama ilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni;<br>c) Kufanya uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha kwa kila zabuni inayokidhi matakwa (yaani, tathmini ya bei ya ununuzi, gharama za uendeshaji, gharama za matengenezo na gharama za nje) kama ilivyoonyeshwa kwenye Mwongozo huu;<br>d) Kutathmini zabuni kulingana na vigezo vya tathmini vilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni;<br>e) Kuhakiki masharti ya uendelevu yaliyotolewa kwenye nyaraka za zabuni kama vile sera, uthibitisho na viwango vinavyotolewa na vyombo husika; na<br>f) Kupendekeza zabuni yenye faida zaidi kwa ajili ya kupewa tuzo iliyopatikana baada ya kufanya uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16. | **Utoaji wa Tuzo** | 16.1 | Taasisi nunuzi inapaswa kutoa tuzo ya mkataba kwa mzabuni aliyekidhi vigezo vya uendelevu vilivyoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni. |
| | | 16.2 | Pale inapohusika, taasisi nunuzi inapaswa kufanya uhakiki wa baada ya tathmini kwa mzabuni aliyependekezwa kupewa tuzo ili kuthibitisha uwezo wake wa kutimiza matakwa ya uendelevu. |
| 17. | **Usimamizi wa Mikataba** | 17.1 | Wakati wa utekelezaji wa mkataba, wasimamizi wa mradi/wasimamizi wa mkataba wanapaswa kuhakikisha kuwa mkataba unasimamiwa ipasavyo na masharti ya uendelevu yaliyomo kwenye mkataba yanatekelezwa kikamilifu na ipasavyo na endapo kutatokea uvunjaji wowote, hatua dhidi ya muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma zichukuliwe kulingana na vigezo na masharti ya mkataba. Masharti yafuatayo ya uendelevu yanapaswa kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa mkataba:<br>(a) Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii utakuwa miongoni mwa nyaraka muhimu za mkataba kwa Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma ili kuwajibika kutekeleza hatua za kimazingira na kijamii walizokubaliana. Mpango huu utajumuisha hatua zitakazochukuliwa na Muuzaji wa bidhaa /Mkandarasi/Mtoa Huduma wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa mkataba ili kuondoa au kudhibiti athari hasi za Kimazingira na Kijamii au kuzipunguza hadi kufikia viwango vinavyokubalika; pamoja na vitendo vinavyohitajika kutekeleza hatua hizo; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (b) Mpango wa usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi utakuwa miongoni mwa nyaraka muhimu za kataba kwa Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma ili kuwajibika kutekeleza walivyokubaliana. Mpango huu utajumuisha hatua za kuchukua na Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa mkataba ili kuondoa au kudhibiti hatari hasi za usalama na afya mahali pa kazi ili kupuzipunguza kwa viwango vinavyokubalika, pamoja na vitendo vinavyohitajika kutekeleza hatua hizo;<br><br>(c) Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma katika mkataba mdogo atawajibika kuzingatia masharti ya kimazingira na kijamii yanaendana na shughuli wanazotekeleza;<br><br>(d) Meneja wa Mradi/Meneja wa Mkataba atatekeleza yafuatayo kuhusiana na masharti ya kimazingira na kijamii:-<br><br>(i) Kufuatilia afya, hali ya kazi, na muda wa kazi wa wafanyakazi;<br><br>(ii) Kuhakikisha mafunzo ya utambulisho kuhusu Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia / Ukatili wa Kijinsia, ubaguzi, ajira ya kulazimishwa, na ajira ya watoto yanatolewa na Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma;<br><br>(iii) Kutoa maelekezo kwa Muuzaji wa bidhaaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kupunguza hatari yoyote inayoathiri usalama wa maisha, bidhaa, kazi za ujenzi au huduma, au mali inayozunguka eneo la mradi;<br><br>(iv) Kufanya mapitio ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii kufuatia mapitio ya mara kwa mara ya Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa huduma, si chini ya kila miezi sita;<br><br>(v) Kupokea matamko kutoka kwa Wauzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Watoa Huduma wenye mikataba midogo kuhusiana na Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia / Ukatili wa Kijinsia (mfano, kuthibitisha kuwa hawajawahi kuondolewa kutokana na kutokidhi);<br><br>(vi) Kufanya mapitio ya ripoti ya tathmini ya hatari za afya na usalama, sera, na Mpango wa Usimamizi wa Usalama na Afya yaliyotayarishwa mahususi kwa ajili ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma;<br><br>(vii) Kuhakikisha kwamba minyororo ya ugavi ya wakandarasi, wauzaji wa bidhaa na watoa huduma inaendana na masharti ya uendelevu;<br><br>(viii) Kukubaliana na hatua za Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa huduma kufidia madhara yoyote kwa mazingira, mali na/au usumbufu kwa watu ndani au nje ya eneo la mradi unaotokana na shughuli za Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa huduma; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | (ix) Kupokea taarifa kuhusu tuhuma, tukio au ajali yoyote ambayo ina au inayoweza kusababisha madhara makubwa kwa mazingira, jamii zilizoathirika, umma, watumishi wa Mwajiri, au watumishi wa Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma;<br><br>(x) Kumtaka Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma kumuondoa mtu yeyote ambaye mienendo yake inahatarisha usalama, afya, au uhifadhi wa mazingira, au anayekiuka Kanuni ya Maadili;<br>(xi) Kukubali tathmini ya hatari iliyofanywa na Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma kabla ya watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 kuruhusiwa kufanya kazi katika eneo la mradi;<br><br>(xii) Kupokea muhtasari wa kila mwezi kutoka kwa Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma kuhusu kumbukumbu za ajira za wafanyakazi, ikijumuisha majina, umri, jinsia, saa walizofanya kazi na mishahara waliolipwa wafanyakazi wote, na kufanya mapitio dhidi ya masharti yaliyopo ya ajira chini ya mkataba; na<br><br>(xiii) Pale inapohitajika, kuielimisha jamii inayozunguka mradi na timu ya mradi kuhusu masuala ya uendelevu.<br><br>(e) Kipindi cha maandalizi ya utekelezaji wa mradi kitumiwe na Taasisi Nunuzi kuthibitisha kuwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Wauzaji wa bidhaa/Wakandarasi/Watoa Huduma, wakandarasi wadogo na watumishi wao wanafahamu hatari zinazohusiana na mazingira na jamii pamoja na wajibu wao wa kimkataba. Kipindi hiki pia kitumiwe kuendeleza mahusiano (ikiwa inafaa) na taasisi za ukaguzi wa kazi kujadili mbinu za muuzaji wa bidhaa/mkandarasi/mtoa huduma za usimamizi wa wafanyakazi. Muuzaji wa bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma pia anaweza kushirikiana na mamlaka za eneo husika kuhusu masuala ya kukabili majanga na maandalizi ya dharura. |
| 18. | **Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo** | 18.1 | Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu au pale kutakapokuwa na uhitaji. |

# ORODHA YA MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

### A. Gharama ya Mzunguko wa Maisha (LCC)

1.5 Gharama za Mzunguko wa Maisha ni muhimu ili kuonyesha kwamba michakato na maamuzi ya ununuzi yanapaswa kwenda zaidi ya kuzingatia tu bei ya ununuzi wa bidhaa au huduma. Bei ya ununuzi haiakisi faida za kifedha na zisizo za kifedha zinazotolewa na mali zinazopendelewa kimazingira na kijamii ambazo hupatikana wakati wa hatua za uendeshaji na matumizi katika mzunguko wa maisha wa mali.

1.6 Taasisi Nunuzi inapaswa kuangalia gharama ya bidhaa inayopatikana katika kipindi chote cha mzunguko wa maisha ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zitakazonunuliwa.

1.7 Pale ambapo Taasisi Nunuzi zinakosa utaalam wa kufanya uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha, wanaweza kualika wataalam wakati wa mchakato wa tathmini.

1.8 Kwa madhumuni ya kufanya uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha kwa ufanisi, Taasisi Nunuzi zitawataka wazabuni kuwasilisha, sambamba na bei ya ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma mgawanyo wa kina wa gharama za uendeshaji, maisha marefu ya bidhaa (muda wa uhai), na gharama za mwisho wa matumizi (kama vile ubomoaji na uondoshaji) kwa kipindi maalum (idadi ya miaka) wakati wa mchakato wa kuwasilisha zabuni, kwa kutumia muundo uliowekwa kwenye **Jedwali Na. 1** hapa chini:

**JEDWALI LA KWANZA**: Muundo wa Mchanganuo wa Gharama za Mzunguko wa Maisha *(utawasilishwa na wazabuni)*

| Mchanganuo wa Gharama za Bidhaa, Kazi za ujenzi au Huduma Zitakazonunuliwa | |
|---|---|
| Bei ya ununuzi (bei ya zabuni): | |

| Muda wa matumizi (*idadi ya miaka*): | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. Gharama za Matengenezo** *(Jumla ya matengenezo yanayohitajika kwa miaka 5 au muda wa matumizi)* | | | | | |
| Kipengele | Mwaka wa 1 | Mwaka wa 2 | Mwaka wa 3 | Mwaka wa 4 | Mwaka wa 5 |
| Idadi ya Matengenezo | | | | | |
| Gharama ya utengenezaji mmoja | | | | | |
| B. Gharama za uendeshaji *(Gharama za uendeshaji zinazohitajika kwa miaka 5 au muda wa matumizi)* | | | | | |
| Kipengele | Mwaka wa 1 | Mwaka wa 2 | Mwaka wa 3 | Mwaka wa 4 | Mwaka wa 5 |
| Gharama ya uendeshaji 1 | | | | | |
| Idadi ya vipengele | | | | | |
| Gharama kwa kila kipengele | | | | | |
| | | | | | |
| Gharama ya uendeshaji 2 | | | | | |
| Idadi ya vipengele | | | | | |
| Gharama kwa kila kipengele | | | | | |
| | | | | | |
| Gharama ya uendeshaji | | | | | |
| Idadi ya vipengele | | | | | |
| Gharama kwa kila kipengele | | | | | |
| C. **Gharama za Nje** *(Jumla ya hewa ya ukaa inayozalishwa kwa miaka 5 au muda wa matumizi)* | | | | | |
| Kipengele | Mwaka wa 1 | Mwaka wa 2 | Mwaka wa 3 | Mwaka wa 4 | Mwaka wa 5 |
| Uzalishaji wa hewa ukaa kwa mwaka kulingana na vigezo msawazo vya bidhaa | N1 | N2 | N3 | N4 | N5 |

1.9 Katika kukotoa gharama za mzunguko wa maisha, Taasisi Nunuzi zitazingatia mwongozo wa ukokotoaji katika **Jedwali la Pili** hapa chini:

**Jedwali la pili: Mwongozo wa ukokotoaji wa gharama za mzunguko wa maisha**

| |
|---|
| Uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha<br><br>Mambo ya kuzingatia katika uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha: -<br><br>a) Gharama za ununuzi na gharama zote zinazoambatana nazo kama vile uwasilishaji, usimikaji, uanzishaji wa kifaa, na bima.<br><br>b) Gharama za uendeshaji, ikijumuisha gharama za matumizi kama vile nishati na maji pamoja na gharama za matengenezo.<br><br>c) Gharama za mwisho wa matumizi ya kifaa kama vile uondoaji, urejeleaji au ukarabati na uondoaji rasmi wa kifaa.<br><br>d) Kudumu kwa bidhaa (umri wa matumizi ya bidhaa) na muda wa dhamana wa rasilimali husika.<br><br>e) Upatikanaji na Uhakika wa Taarifa: Ukokotoaji wa gharama za mzunguko wa maisha unahitaji taarifa za gharama zitakazotokea siku zijazo kama ilivyoelezwa katika kipengele (a–d), ambapo kuna kipengele cha kutotabirika. Hivyo, wazabuni wanapaswa kuombwa kuwasilisha taarifa za kina juu ya makadirio ya gharama. Kwa gharama za baadaye ambazo ziko chini ya udhibiti wa mzabuni (kwa mfano, kama wanahusika na matengenezo au uondoaji), viwango vya juu vya gharama zinazotarajiwa vinaweza kuwekwa. Kwa kufanya hivyo, uhakika mkubwa unaweza kupatikana katika ukokotoaji wa gharama za mzunguko wa maisha<br><br>f) Kiwango cha punguzo: Gharama za mzunguko wa maisha huzingatia thamani ya fedha kwa wakati, yaani kiasi cha fedha kilichopo leo kina thamani kubwa zaidi kuliko kiasi kilekile kitakapopatikana baadaye kwa kuwa kinaweza kupata riba kadiri muda unavyopita. Kiwango cha punguzo kwa kawaida hutumika kuwa kiwango cha taifa cha riba kinachotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Kwa kukitumia kwenye gharama za baadaye, husaidia kubaini thamani ya sasa ya gharama hizo za baadaye. Kwa njia hii, kulinganisha gharama za sasa na za baadaye kunaweza kufanywa, jambo ambalo ni muhimu katika ulinganifu wa gharama za mzunguko wa maisha.<br><br>Mfano wa matumizi ya gharama za mzunguko wa maisha katika ununuzi wa mashine ya uchapishaji kazi nzito) (*Ni mfano tu; unaweza kuongeza gharama zingine za uendeshaji inapobidi*) |

<table>
<tr><td colspan="6">Njia za kukokotoa Gharama za Mzunguko wa Maisha ya Mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito zilizoelezwa hapa chini itatumika na Taasisi nunuzi katika kutathmini zabuni. Njia hii imeandaliwa ikizingatia awamu mbalimbali za mzunguko wa maisha wa mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Bei ya ununuzi (kama ilivyowasilishwa na mzabuni)</td><td>(I)</td></tr>
<tr><td colspan="5">Muda wa matumizi ya mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito (kama ilivyoelezwa na taasisi nunuzi kwa malengo ya gharama za mzunguko wa maisha au kutumia Sheria na Kanuni za Fedha)</td><td>Miaka 5</td></tr>
<tr><td colspan="5">Kiwango cha punguzo (i) (kama ilivyotolewa na Banki Kuu ya Tanzania)</td><td>Weka kiwango</td></tr>
<tr><td colspan="6">Gharama za Matengenezo (Jumla ya matengenezo kwa kipindi cha miaka 5 (muda wa matumizi)</td></tr>
<tr><td>Kipengele</td><td>Mwaka 1</td><td>Mwaka 2</td><td>Mwaka 3</td><td>Mwaka 4</td><td>Mwaka 5</td></tr>
<tr><td>Idadi ya matengenezo (N) (kama alivyowasilishwa mzabuni)</td><td>N1</td><td>N2</td><td>N3</td><td>N4</td><td>N5</td></tr>
<tr><td>Gharama ya tengenezo moja (C)</td><td>C1</td><td>C2=C1(1+i)</td><td>C3=C2(1+i)</td><td>C4=C3(1+i)</td><td>C5=C4(1+i)</td></tr>
<tr><td>Gharama ya matengenezo kwa mwaka (N x C)</td><td>N1C1</td><td>N2C2</td><td>N3C3</td><td>N4C4</td><td>N5C5</td></tr>
<tr><td colspan="5">Jumla ya gharama za matengenezo ∑NiCi</td><td>(II)</td></tr>
<tr><td colspan="6">Gharama za Wino</td></tr>
<tr><td>Kipengele</td><td>Mwaka 1</td><td>Mwaka 2</td><td>Mwaka 3</td><td>Mwaka 4</td><td>Mwaka 5</td></tr>
<tr><td>Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka (N)</td><td>N1</td><td>N2</td><td>N3</td><td>N4</td><td>N5</td></tr>
<tr><td>Gharama ya wino mmoja (C)</td><td>C1</td><td>C2=C1(1+i)</td><td>C3=C2(1+i)</td><td>C4=C3(1+i)</td><td>C5=C4(1+i)</td></tr>
<tr><td>Gharama za wino kwa mwaka (N x C)</td><td>N1C1</td><td>N2C2</td><td>N3C3</td><td>N4C4</td><td>N5C5</td></tr>
</table>

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya gharama za wino ∑NiCi | | | | | (III) |
| Gharama za Nje (mfano: Uzalishaji wa hewa ukaa) | | | | | |
| Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka (N) *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | N1 | N2 | N3 | N4 | N5 |
| Idadi ya machapisho/nakala kwa kila wino (P) *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | P1 | P2 | P3 | P4 | P5 |
| Gharama ya utoaji hewa ukaa/kaboni kwa kila chapisho/nakala *(Tumia viwango vya kimataifa vinavyowezeka 3-4g)* | C1 | C2 | C3 | C4 | C5 |
| Hewa ukaa inayozalishwa kwa mwaka | N1P1C1 | N2P2C2 | N3P3C3 | N4P4C4 | N5P5C5 |
| Jumla ya gharama za nje ∑NiPiCi | | | | | (IV) |
| Gharama za Mzunguko wa Maisha (ya Mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito kwa miaka 5) | | | | | I+II+III+IV |

**MFANO WA HESABU HALISI**

Mfano uliotolewa katika Mwongozo huu unahusisha zabuni tatu zilizopokelewa kutoka kwa wazabuni watatu kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito. Mzabuni A aliwasilisha bei ya zabuni ya Ths 230,000,000, Mzabuni B aliwasilisha bei ya zabuni ya Ths 210,000,000, na Mzabuni C aliwasilisha bei ya zabuni ya Ths 250,000,000. Kufuatia uchambuzi wa Gharama za Mzunguko wa Maisha kama ilivyoelezwa hapa chini, bei ya Gharama za Mzunguko wa Maisha ilikuwa: Ths 246,394,498.50 kwa Mzabuni A, Ths 247,108,227.89 kwa Mzabuni B, na Ths 263,123,932.74 kwa Mzabuni C.

Hivyo, kwa kuzingatia Gharama za Mzunguko wa Maisha kama sehemu ya vigezo vya uendelevu, tuzo ya zabuni itatolewa kwa Mzabuni A, hata kama bei yake ya awali ya ununuzi ilikuwa juu kuliko ile ya Mzabuni B.

**Jedwali la Tatu:** Mfano wa ukokotoaji wa gharama za mzunguko wa maisha

| A | B | C | D | E | F | G |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mzabuni A | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | Bei ya Ununuzi (*kama ilivyowasilishwa na Mzabuni)* | | | | | 230,000,000.00 |
| 5. | Muda wa matumizi | | | | | 5 |
| 6. | Kiwango cha punguzo (i) (kama ilivyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania) | | | | | 7% |
| 7. | Gharama za Matengenezo (*Jumla ya matengenezo kwa kipindi cha miaka 5 (muda wa matumizi)* | | | | | |
| 8. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 9. | Idadi ya matengenezo (N) *(kama alivyowasilishwa mzabuni)* | 1 | 2 | 2 | 3 | 3 |
| 10. | Gharama ya tengenezo moja (C) | 650,000.00 | 695,500.00 | 744,185.00 | 796,277.95 | 852,017.41 |
| *11.* | *Fomyula* | #N/A | =C10*(1+$G$6) | =D10*(1+$G$6) | =E10*(1+$G$6) | =F10*(1+$G$6) |
| 12. | Gharama ya matengenezo kwa mwaka | 650,000.00 | 1,391,000.00 | 1,488,370.00 | 2,388,833.85 | 2,556,052.22 |
| *13.* | *Fomyula* | =C9*C10 | =D9*D10 | =E9*E10 | =F9*F10 | =G9*G10 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Jumla ya gharama za matengenezo ∑NiCi…………………………………… | | | | | 8,474,256.07 |
| 15. | Cost of Cartridge (Toner) | | | | | |
| 16. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 17. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyoainishwa na Taasisi nunuzi)* | 3 | 3 | 5 | 5 | 8 |
| 18. | Gharama ya wino mmoja | 270,000.00 | 288,900.00 | 309,123.00 | 330,761.61 | 353,914.92 |
| *19.* | *Fomyula* | #N/A | =C18*(1+$G$6) | =D18*(1+$G$6) | =E18*(1+$G$6) | =F18*(1+$G$6) |
| 20. | Gharama za wino kwa mwaka | 810,000.00 | 866,700.00 | 1,545,615.00 | 1,653,808.05 | 2,831,319.38 |
| *21.* | *Fomyula* | =C17*C18 | =D17*D18 | =E17*E18 | =F17*F18 | =G17*G18 |
| 22. | Jumla ya gharama za wino ∑NiCi…………………………………… | | | | | 7,707,442.43 |
| 23. | Gharama za Nje (mfano: Uzalishaji wa hewa ukaa) | | | | | |
| 24. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 25. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 2 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| 26. | Idadi ya machapisho/nakala kwa kila wino *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 3800 | 3800 | 3800 | 3800 | 3800 |
| 27. | Gharama ya utoaji hewa ukaa/kaboni kwa kila chapisho/nakala *(Tumia viwango vya kimataifa vinavyowezeka 3-4g)* | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| 28. | Hewa ukaa inayozalishwa kwa mwaka | 22,800.00 | 34,200.00 | 34,200.00 | 60,800.00 | 60,800.00 |
| *29.* | *Fomyula* | =C25*C26*C27 | =D25*D26*D27 | =E25*E26*E27 | =F25*F26*F27 | =G25*G26*G27 |
| 30. | Jumla ya gharama za nje ∑NiPiCi…………………………………… | | | | | 212,800.00 |
| 31. | Gharama za Mzunguko wa Maisha (ya Mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito kwa miaka 5) kwa Mzabuni A | | | | | 246,394,498.50 |
| *32.* | *Fomyula* | | | | | =G4+G14+G22+G30 |
| **33.** | Mzabuni B | | | | | |
| 34. | | | | | | |
| 35. | Bei ya Ununuzi (*kama ilivyowasilishwa na Mzabuni)* | | | | | 210,000,000.00 |
| 36. | Muda wa matumizi | | | | | 5 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 37. | Kiwango cha punguzo (i) (kama ilivyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania) | | | | | 7% |
| 38. | Gharama za Matengenezo (*Jumla ya matengenezo kwa kipindi cha miaka 5 (muda wa matumizi)* | | | | | |
| 39. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 40. | Idadi ya matengenezo (N) *(kama alivyowasilishwa mzabuni)* | 2 | 2 | 3 | 4 | 4 |
| 41. | Gharama ya tengenezo moja (C) | 1,000,000.00 | 1,070,000.00 | 1,144,900.00 | 1,225,043.00 | 1,310,796.01 |
| *42.* | *Fomyula* | #N/A | =C41*(1+$G$6) | =D41*(1+$G$6) | =E41*(1+$G$6) | =F41*(1+$G$6) |
| 43. | Gharama ya matengenezo kwa mwaka | 2,000,000.00 | 2,140,000.00 | 3,434,700.00 | 4,900,172.00 | 5,243,184.04 |
| *44.* | *Fomyula* | =C40*C41 | =D40*D41 | =E40*E41 | =F40*F41 | =G40*G41 |
| 45. | Jumla ya gharama za matengenezo ∑NiCi…………………………………… | | | | | 17,718,056.04 |
| 46. | Cost of Cartridge (Toner) | | | | | |
| 47. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 48. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyoainishwa na Taasisi nunuzi)* | 5 | 6 | 7 | 8 | 10 |
| 49. | Gharama ya wino mmoja | 450,000.00 | 481,500.00 | 515,205.00 | 551,269.35 | 589,858.20 |
| *50.* | *Fomyula* | #N/A | =C49*(1+$G$6) | =D49*(1+$G$6) | =E49*(1+$G$6) | =F49*(1+$G$6) |
| 51. | Gharama za wino kwa mwaka | 2,250,000.00 | 2,889,000.00 | 3,606,435.00 | 4,410,154.80 | 5,898,582.05 |
| *52.* | *Fomyula* | =C48*C49 | =D48*D49 | =E48*E49 | =F48*F49 | =G48*G49 |
| 53. | Jumla ya gharama za wino ∑NiCi…………………………………… | | | | | 19,054,171.85 |
| 54. | Gharama za Nje (mfano: Uzalishaji wa hewa ukaa) | | | | | |
| 55. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 56. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 4 | 4 | 6 | 6 | 10 |
| 57. | Idadi ya machapisho/nakala kwa kila wino *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 2800 | 2800 | 2800 | 2800 | 2800 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 58. | Gharama ya utoaji hewa ukaa/kaboni kwa kila chapisho/nakala *(Tumia viwango vya kimataifa vinavyowezeka 3-4g)* | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 |
| 59. | Hewa ukaa inayozalishwa kwa mwaka | 44,800.00 | 44,800.00 | 67,200.00 | 67,200.00 | 112,000.00 |
| *60.* | *Fomyula* | =C56*C57*C58 | =D56*D57*D58 | =E56*E57*E58 | =F56*F57*F58 | =G56*G57*G58 |
| 61. | Jumla ya gharama za nje ∑NiPiCi…………………………………… | | | | | 336,000.00 |
| 62. | Gharama za Mzunguko wa Maisha (ya Mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito kwa miaka 5) kwa Mzabuni B | | | | | 247,108,227.89 |
| *63.* | *Fomyula* | | | | | =G35+G45+G53+G61 |
| 64. | Mzabuni C | | | | | |
| 65. | | | | | | |
| 66. | Bei ya Ununuzi (*kama ilivyowasilishwa na Mzabuni)* | | | | | 250,000,000.00 |
| 67. | Muda wa matumizi | | | | | 5 |
| 68. | Kiwango cha punguzo (i) (kama ilivyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania) | | | | | 7% |
| 69. | Gharama za Matengenezo (*Jumla ya matengenezo kwa kipindi cha miaka 5 (muda wa matumizi)* | | | | | |
| 70. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 71. | Idadi ya matengenezo (N) *(kama alivyowasilishwa mzabuni)* | 2 | 2 | 3 | 3 | 3 |
| 72. | Gharama ya tengenezo moja (C) | 600,000.00 | 642,000.00 | 686,940.00 | 735,025.80 | 786,477.61 |
| *73.* | *Fomyula* | #N/A | =C72*(1+$G$6) | =D72*(1+$G$6) | =E72*(1+$G$6) | =F72*(1+$G$6) |
| 74. | Gharama ya matengenezo kwa mwaka | 1,200,000.00 | 1,284,000.00 | 2,060,820.00 | 2,205,077.40 | 2,359,432.82 |
| *75.* | *Fomyula* | =C71*C72 | =D71*D72 | =E71*E72 | =F71*F72 | =G71*G72 |
| 76. | Jumla ya gharama za matengenezo ∑NiCi…………………………………… | | | | | 9,109,330.22 |
| 77. | Cost of Cartridge (Toner) | | | | | |
| 78. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 79. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyoainishwa na Taasisi nunuzi)* | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| 80. | Gharama ya wino mmoja | 170,000.00 | 181,900.00 | 194,633.00 | 208,257.31 | 222,835.32 |
| *81.* | *Fomyula* | #N/A | =C80*(1+$G$6) | =D80*(1+$G$6) | =E80*(1+$G$6) | =F80*(1+$G$6) |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 82. | Gharama za wino kwa mwaka | 510,000.00 | 545,700.00 | 778,532.00 | 833,029.24 | 891,341.29 |
| *83.* | *Fomyula* | =C79*C80 | =D79*D80 | =E79*E80 | =F79*F80 | =G79*G80 |
| 84. | Jumla ya gharama za wino ∑NiCi…………………………………… | | | | | 3,558,602.53 |
| 85. | Gharama za Nje (mfano: Uzalishaji wa hewa ukaa) | | | | | |
| 86. | Kipengele | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 | Mwaka 4 | Mwaka 5 |
| 87. | Idadi ya wino zinazohitajika kwa mwaka *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 4 | 4 | 6 | 6 | 10 |
| 88. | Idadi ya machapisho/nakala kwa kila wino *(kama ilivyowasilishwa na mzabuni)* | 3800 | 3800 | 3800 | 3800 | 3800 |
| 89. | Gharama ya utoaji hewa ukaa/kaboni kwa kila chapisho/nakala *(Tumia viwango vya kimataifa vinavyowezeka 3-4g)* | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 |
| 90. | Hewa ukaa inayozalishwa kwa mwaka | 60,800.00 | 60,800.00 | 91,200.00 | 91,200.00 | 152,000.00 |
| *91.* | *Fomyula* | =C87*C88*C89 | =D87*D88*D89 | =E87*E88*E89 | =F87*F88*F89 | =G87*G88*G89 |
| 92. | Jumla ya gharama za nje ∑NiPiCi…………………………………… | | | | | 456,000.00 |
| 93. | Gharama za Mzunguko wa Maisha (ya Mashine ya uchapishaji/kudurufu kazi nzito kwa miaka 5) kwa Mzabuni C | | | | | 263,123,932.74 |
| *94.* | *Fomyula* | | | | | =G66+G76+G84+G92 |